

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SIMU 0789 864674  
0719 003505

SHULE YA SEKONDARI NARUNGOMBE  
S. L. P 84  
RUANGWA.

KUMB NO NASECO/ADM/S.3906/.....

TAREHE .....

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI  
.....

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA  
MWAKA.....KATIKA SHULE YA SEKONDARI NARUNGOMBE**

Tafadhali rejea kichwa cha somo hapo juu.

Napenda kuchukua nafasi hii kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Narungombe. Hivyo ninakupongeza sana kwa mwanao kufanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba mwaka ..... shule ya sekondari Narungombe ni ya kutwa na ipo katika kijiji cha Narungombe kata ya Narungombe. Shule itafunguliwa tarehe ..... hivyo bila kuchelewa unatakiwa kumleta mtoto wako shuleni mapema. Kinyume na hapo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako. Aidha unatakiwa kutekeleza hili kwa kuzingatia kauli mbiu ya Mhe Rais ya kuleta maendeleo ya nchi ya **HAPA KAZI TU.**

Aidha maelezo ya fomu hii yanazingatia utekelezaji wa waraka wa elimu Na 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimu Msingi na Sekondari bila malipo. Hivyo Mzazi/Mlezi unatakiwa kufanya yafuatayo ili mtoto wako aweze kupata elimu ya sekondari na pia kuonyesha ushirikiano na shule na serikali kwa ujumla. Unatakiwa kutekeleza jukumu lako kama Mzazi/Mlezi kwa kumuandaa mtoto wako kwa vitu vya msingi kama:-

**A. WAVULANA**

- i. Suruali ndefu zisizobana (modo) rangi ya khaki zenye mikunjo chini(turnup)
- ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi aina ya tomato
- iii. Soksi nyeupe mbili
- iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na Kamba au gidamu
- v. Mkanda mweusi wa ngozi wenye bangozi ndogo
- vi. Singilendi nyeupe mbili.
- vii. Sweta yenye rangi ya bendera ya Taifa.
- viii. Jezi nyekundu yenye mistari nyeupe Adidas, viatu vya michezo (njumu) na soksi ndefu nyekundu.

**B. WASICHANA**

- i. Siketi mbili ndefu (rangi ya kijani)
- ii. Mashati mawili meupe ya tomato
- iii. Soksi nyeupe mbili
- iv. Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba au gidamu jozi mbili
- v. Singilendi nyeupe mbili.
- vi. Kwa wale wanaovaa hujabu zifunike viwiko vya mkono

- vii. Sweta yenye rangi ya bendera ya Taifa.
- viii. Jezi ya njano yenye mistari ya kijani pamoja na track ya njano na raba

### **C. VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

- i. Daftari counter book quire 2 idadi kumi(10)
- ii. Begi la kubebea daftari moja(1) mifuko ya Rambo hairuhusiwi
- iii. Mkebe uliojaa vifaa vya kujifunzia mmoja(1), kalamu,rula na penseli
- iv. Kamusi ya kiingereza na Kiswahili.

### **D. VIFAA VYA SHULE**

- i. Jembe jipya moja (1) lenye mpini
- ii. Fyekeo moja (1) iliyonolewa
- iii. ndoo ndogo moja(1).
- iv. Panga moja (1)
- v. Fagio la chelewa la wima moja (1)

NB: aidha tambua kuwa ni marufuku mmwanafunzi kuvaa ndara, makatambuga (matairi) shuleni na endapo mtoto wako atakutwa amevaa basi atachukuliwa hatua za kinidhamu mara moja.

Tambua kuwa serikali imesema imesema elimu bure ila mzazi/mlezi unatakiwa kugharamia matibabu kwa mtoto wako kwa muda wote pale zahanati ya Narungombe, Ruangwa na katika hospitali nyinginezo. Hivyo utamsaidia mtoto wako kuwa na afya njema na ataweza kumudu masomo yake vizuri.

Kumbuka kumleta mwanao shuleni mapema iwezekanavyo na endapo hautamleta mtoto shuleni utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kupelekwa mahakamani kwa kutotimiza wajibu wako kama Mzazi/Mlezi pia kumnyima mtoto haki yake ya kupata elimu ya sekondari. Pia tambua kuwa utakuwa umetenda kosa la jinai hivyo utastahili kutumikia kifungo cha kwenda jela kwa mujibu wa sheria za Nchi.

Katika fomu hii naambatanisha na nakala ya sheria za shule ambazo mwanao na wewe mzazi/mlezi mnatakiwa kuzisoma na kuzielewa pia nakuambatanishia na fomu maalum ambayo mwanao atapaswa kupimwa na daktari katika hospitali ya wilaya ya Ruangwa kujua afya yake.

Mwisho nakutaki maandalizi mema. Karibu sana shule ya sekondari Narungombe.

.....  
PAUL S. MCHANGA  
MKUU WA SHULE

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU  
KUSIMAMISHWA SHULE KWA MWANAFUNZI**

- a. Wizi
- b. Uasherati na ushoga
- c. Ubakaji
- d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi nk
- e. Kupigana au kupiga
- f. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- g. Kudharau bendera ya Taifa
- h. Kuwa mjamzito/kupata mimba
- i. Kuoja au kuolewa
- j. Kutoa mimba
- k. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
- l. Kukataa adhabu kwa makusudi
- m. Kuwa na simu ya mkononi
- n. Utoro unaozidi siku 90 (miezi mitatu)

NARUNGOMBE SECONDARY SCHOOL  
P. O. BOX 84  
RUANGWA  
DATE .....

REF. NO.....

THE MEDICAL OFFICER

.....  
.....  
.....

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF MR/MISS.....

Please. Examine the above named pupil and give us regarding his/her suitability for secondary school studies.

1. Pupil's full name .....
2. Blood .....
3. Stool .....
4. T.B Test .....
5. Syphilis test .....
6. Urine Examination .....
7. Eye test .....
8. Chest .....
9. Ear .....
10. Spleen .....
11. Abdomen test .....
12. Pregnant test (girls only) .....

I certify that the above pupil is suitable/unsuitable for studies

If unsuitable please give reasons

.....  
.....  
.....

Name of medical Officer .....

Signature of Medical Officer .....

Date .....

Official stamp .....